

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

CHUO CHA VIWANDA VYA MISITU, MOSHI

**NAFASI ZA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA TEKNOLOJIA YA VIWANDA VYA MISITU KWA
MWAKA WA MASOMO 2020/2021**

Mkuu wa Chuo cha Viwanda vya Misitu kilichopo Moshi anakaribisha maombi ya kujunga na chuo kwa kozi za Astashahada (Cheti) na Stashahada (Diploma) kwa mwaka wa masomo 2020/2021.

A. Kozi zinazotolewa:

- i. Astashahada ya Awali ya Teknolojia ya Viwanda vya Misitu (NTA – Level 4) Mafumzo ya mwaka mmoja (1);
- ii. Astashahada ya Teknolojia ya Viwanda vya Misitu (NTA – Level 5) Mafunzo ya mwaka mmoja; (1);
- iii. Stashahada ya Teknolojia ya Viwanda vya Misitu (NTA – Level 6) Mafunzo ya mwaka mmoja (1);

B. Sifa za mwombaji:

- i. **Astashahada ya awali ya Teknolojia ya Viwanda vya Misitu;**
 -) Mwombaji awe na cheti cha kuhitimu elimu ya sekondari na ufaulu wa angalau alama **D** katika masomo manne;
 -) Masomo mawili kati ya hayo aliyofaulu yawe aidha Biolojia, Kemia, Fizikia Hesabu au Jiografia;
 -) Masomo mengine mawili kati ya hayo aliyofaulu yawe siyo ya dini. Ufaulu wa somo la kiingereza utakuwa kipaumbele cha ziada katika uchaguzi.
- ii. **Astashahada ya Teknolojia ya Viwanda vya Misitu;**
 -) Mwombaji awe na cheti cha kuhitimu Astashahada ya awali ya Teknolojia ya Viwanda vya Misitu au Astashahada ya awali ya Ufugaji Nyuki au fani nyingine inayolandana na hizo kutoka chuo chochote kinachotambulika na Baraza la Elimu ya Ufundji (NACTE);

AU

- J Mwombaji awe na cheti cha kuhitimu elimu ya juu ya sekondari na awe na amesoma michepuo ya sayansi na kufaulu katika masomo mawili kwa alama ya **E (Principal)** na **S (Subsdiary)**;

iii. **Stashahada ya Teknolojia ya Misitu;**

- J Mwombaji awe na cheti cha kuhitimu Astashahada ya Teknolojia ya Viwanda vya Misitu au fani nyingine ya sayansi inayoendana na hizo kutoka chuo chochote kinachotambulika na Baraza la Elimu ya Ufundi(NACTE);

C. Jinsi ya Kutuma maombi:

- I. Mwombaji atatakiwa kujaza fomu, kusaini na kuituma fomu ya maombi ikiwa na vielelezo vyote muhimu. Ada ya maombi ya kujiunga na chuo ni Shilingi za Kitanzania 10,000/= (elfu kumi) kwa Watanzania na Dola za Kimarekani 20.00 kwa wasio Watanzania;
- II. Fomu za maombi zinapatikana Chuo cha Viwanda vya Misitu, Moshi na kupitia tovuti ya chuo [<http://www.fiti.ac.tz>];
- III. Maombi yote yaambatanishwe na vivuli vya vyeti halisi na taarifa za matokeo katika lugha ya Kiingereza. Endapo mwombaji atakuwa na Ufadhilli, uthibitisho wa maandishi kuhusu Ufadhilli huo utahitajika;
- IV. Mwombaji anatakiwa kulipa ada ya maombi kupitia **control number**,
- V. Ili kupata **control number** au kupata ufanuzi wa jinsi ya kujiunga na chuo, mwombaji awasiliane na Afisa udahili wa chuo kwa namba +255755771852 **au** +255717085141;

D. Tahadhari

- I. Kwa yeoyote ambaye hatazingatia utaratibu uliotajwa hapo juu, maombi yake hayatafikiriwa. Aidha , mwombaji atakayewasilisha hati za kughushi atachukuliwa hatua za kisheria ;
- II. Maombi yote yatumwe kupitia anwani ifuatayo:- **Msajili, Chuo cha Viwanda vya misitu, S.L.P 1925, Moshi** au kupitia email ya info@fiti.ac.tz
- III. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **15 septemba 2020**;

E. Taarifa kwa wataochaguliwa;

- ❖ Majina ya wataochaguliwa pamoja na maelezo ya kujiunga na chuo yatawekwa kwenye tovuti ya Chuo (<http://www.fiti.ac.tz>);